TANGAZO LA SERIKALI NA. 843 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA YITWIMILA "B" YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Yitwimila "B"ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Busega.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba MV248 yenye majira - nukta 553985MS, 9728696KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS165$^0$10'55"MS kwa umbali wa kilomita 2.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV347 yenye majira – nukta 554514MS, 9726695KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS224$^0$31'26"MG kwa umbali wa kilomita 2.02 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV207 yenye majira – nukta 553093MS, 9725251KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS262$^0$2'15"MG kwa umbali wa kilomita 3.10 hadi kwenye alama ya

mpaka ya upimaji namba MV334 yenye majira – nukta 549990MS, 9724774KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea
Kaskazini - Magharibi kufuata Ziwa Victoria hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M325 yenye majira – nukta 548442MS, 9726067KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ54$^{0}$15'56"MS kwa umbali wa kilomita 2.53 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV324 yenye majira – nukta 550492MS, 9727542KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ71$^{0}$43'17"MS kwa umbali wa kilomita 3.67 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*